

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU



## TANGAZO LA KOTESHENI YA UENDESHAJI WA MGAHAWA WA HALMASHAURI (CANTEEN)

**KOTESHENI NA. LGA/090 /2017-18/NCS/02 (Limerudiwa)**

**TAREHE 16/03/2018**

Halmashauri ya wilaya ya Magu inapenda kuwaalika watu Binafsi, Makampuni, Ushirika, Taasisi au Vikundi vya watu vilivyosajiliwa kisheria, wenye nia na uwezo wa kuendesha mgahawa wa halmashauri uliopo makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya Magu.

### **MASHARTI YA ZABUNI:**

1. Mwombaji ni lazima awe na leseni hai ya biashara – ambatanisha kivuli cha leseni.
2. Mwombaji awe amesajiliwa na TIN au VAT – ambatanisha kivuli.
3. Mwombaji aonyeshe vifaa alivyo navyo, idadi ya wafanyakazi na uwezo wao.
4. Mwombaji aonyeshe waziwazi ofisi yake ilipo na uzoefu wa kazi anayoiomba.
5. Kila mwombaji atalipa ada ya maombi ya kotesheni shilingi 50,000.00 (elfu hamsini) ambayo haitarudishwa (non-refundable fee).
6. **Makabrasha ya Kotesheni/zabuni** yanapatikana katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi (PMU) ya Halmashauri ya Wilaya ya Magu .
7. Atakayepata atatakiwa kuingia mkataba na Halmashauri ya wilaya ya Magu.
8. Halmashauri hailazimiki kumkubali au kumktaa mzabuni kwa sababu yoyote ile.
9. Kotesheni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha iliyofungwa ipasavyo (Kwa Lakiri). Juu ya bahasha ionyeshwe jina la Kotesheni na namba ya Kotesheni itumwe kwa Mkurugenzi kwa anuani ifuatayo:-

**Katibu wa bodi ya Zabuni,  
Halmashauri ya Wilaya ya Magu,  
S.L.P. 200, Magu.**

10. Kwa maelezo zaidi kuhusiana na Kotesheni hizi, fika katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Magu zilizopo mjini Magu umuone **Katibu wa Bodi ya zabuni**.
11. Vigezo vya tathmini ya Kotesheni ni kama ilivyoainishwa kwenye tangazo pamoja na kwenye nyaraka za Kotesheni.
12. Mwombaji wa Kotesheni atatakiwa kuwasilisha pamoja na kitabu chake cha Kotesheni kinga ya Kotesheni (Tender Security) kwa njia ya dhamana ya kotesheni kwa ahadi.
13. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya Kotesheni hizo ni Alhamis tarehe 22 Machi 2018 ambayo ndiyo itakuwa siku ya ufunguzi wa Kotesheni hizo saa 5.00 asubuhi, katika ukumbi wa **Halmashauri ya Wilaya ya Magu**. Mwombaji au mwakilishi wake wanakaribishwa katika ufunguzi wa Kotesheni hizo.



Merchades Rusasa

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAGU**